



## **Nilishuhudia swala ya Idd pamoja na Omari bin Khattwab radhi za Allah ziwe juu yake, akasema: Siku mbili hizi alikataza Mtume rehema na amani ziwe juu yake kufunga ndani yake: Siku ya kufungua kwenu kutoka katika swaumu yenu, na siku nyingine ni ile mnayokula katika vichinjwa vyenu**

Kutoka kwa Abuu Ubaidi, mwachwa huru wa bin Azhari, amesema: Nilishuhudia swala ya Idd pamoja na Omari bin Khattwab radhi za Allah ziwe juu yake, akasema: Siku mbili hizi alikataza Mtume rehema na amani ziwe juu yake kufunga ndani yake: Siku ya kufungua kwenu kutoka katika swaumu yenu, na siku nyingine ni ile mnayokula katika vichinjwa vyenu.

[Sahihi] [Wamekubaliana Bukhari na Muslim juu ya usahihi wake]

Alikataza Mtume rehema na amani ziwe juu yake kufunga siku ya Iddil-Fitiri na Iddil-Adh-ha; ama Iddil-Fitiri ni siku ya kufungua kutoka katika swaumu ya mwezi wa Ramadhani, na ama Iddil-Adh-ha ni siku ya kula katika vichinjwa.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/4527>

